

Serikali yaahidi Kupambana na Ukiukwaji wa Maadili nchini.

Serikali ya awamu ya tano inayoongozwa na Mhe. Dkt. John Pombe Magufuli imedhamiria kwa dhati kupambana na vitendo vya ukiukaji wa maadili ikiwemo rushwa na uzembe katika utumishi wa Umma ili kuimarisha uwajibikaji na Utawala Bora nchini.

Kauli hiyo ilitolewa na Waziri wa Katiba na Sheria Mhe. Dkt. Harrison Mwakyembe (Mb) ambaye alikuwa mgeni rasmi katika ufunguzi wa Wiki ya Utoaji Huduma katika Maadhimisho ya Siku ya Maadili, Haki za Binadamu, Uwajibikaji, Utawala Bora na Mapambano dhidi ya Rushwa iliyofanyika katika viwanja vya Mnazi Mmoja jijini Dar es Salaam.

Mhe. Mwakyembe katika hotuba yake alibainisha kwamba katika kulinda maadili nchini Wiki ya Kutoa Huduma kwa Wananchi kutatoa fursa kwa wananchi kuweza kuwasilisha malalamiko na kero zao na serikali itayafanyia kazi kwa haraka na kwa wakati.

Aidha, Mhe. Mwakyembe aliwaasa watanzania kuanzisha kampeni za maadili nchini katika ngazi mbalimbali za jamii kwa kushirikiana na viongozi mbalimbali katika jamii wakiwemo viongozi wa dini ili kuhakikisha maadili yanazingatiwa katika ngazi zote.

Naye Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora Mhe. Angellah Kairuki alisema serikali ya awamu ya tano imejipanga kuhakiki Mali na Madeni ya Viongozi wa umma 500 Tanzania nzima ikilinganishwa na miaka ya nyuma ambapo Sekretarieti ya Maadili ilikuwa ikihakiki viongozi mia moja tu kwa mwaka.

Mhe. Kairuki aliongeza kuwa huu ni mkakati mmoja wapo wa kubaini viongozi wasio waadilifu wanaoficha mali zao. Pia, Mhe. Kairuki alitoa rai kwa watanzania kufichua na kutoa taarifa katika Sekretarieti ya Maadili ya Viongozi wa Umma juu ya viongozi wanaojilimbikizia mali kinyume cha sheria.

Aidha, Mhe. Kairuki alifafanua kuwa Serikali ya awamu ya tano itahakikisha kuwa Misingi ya Maadili na Utawala Bora inazingatiwa ipasavyo katika kuhakikisha kuwa maadili yanaimarika katika jamii. Pia aliongeza kuwa suala la maadili si la serikali pekee bali ni la kila mtu katika jamii na kwamba serikali haitasita kumchukulia hatua kiongozi au mtumishi yeyote wa umma atakayekiuka maadili.

Katika maadhimisho hayo jumla ya Taasisi saba zilishiriki katika kutoa elimu kwa wananchi ikiwemo kupokea malalamiko, maoni na ushauri kutoka kwa wananchi na wadau mbalimbali. Taasisi zilizoshiriki ni pamoja na Sekretarieti ya Maadili ya Viongozi wa Umma, TAKUKURU, Tume ya Haki za Binadamu na Utawala Bora, Menejimenti ya Utumishi wa Umma, PPRA, Tume ya Utumishi wa Umma na Ofisi ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesaba za Serikali.

Wiki ya Kutoa Huduma kwa wananchi katika maadhimisho ya Siku ya Maadili, Haki za Binadamu, Uwajibikaji, Utawala Bora na Mapambano dhidi ya Rushwa inatarajiwa kuhitimishwa rasmi tarehe 10 Desemba, 2016 ambapo itakuwa kilele cha maadhimisho hayo.